
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Taarifa ya ALMA ya Robo Mwaka**
**Robo ya Pili, 2025**

MUUNGANO WA VIONGOZI WA AFRIKA
**KATIKA UDHIBITI WA MALARIA**

# Kadi ya Alama ya Uwajibikaji na Utekelezaji

Ramani inayoonesha mtawanyiko wa maambukizi ya Malaria mwaka 2020 - Tanzania




**Metrics**

| Metrics | | |
|---|---|---|
| **Policy** | | |
| Signed, ratified and deposited the AMA instrument at the AUC | | |
| Malaria activities targeting refugees in Malaria Strategic Plan | | |
| Malaria activities targeting IDPs in Malaria Strategic Plan | | |
| Zero Malaria Starts With Me Launched | | |
| End Malaria Council and Fund Launched | | |
| **Resistance Monitoring, Implementation and Impact** | | |
| Drug efficacy studies conducted since 2019 and data reported to WHO | | |
| Insecticide classes with mosquito resistance in representative sentinel sites confirmed since 2010 | | 4 |
| Insecticide resistance monitored since 2020 and data reported to WHO | | |
| % of vector control in the last year with next generation materials | | 97 |
| ACTs in stock (>6 months stock) | | |
| RDTs in stock (>6 months stock) | ▲ | |
| On track to reduce malaria incidence by at least 75% by 2025 (vs 2015) | | |
| On track to reduce malaria mortality by at least 75% by 2025 (vs 2015) | | |
| **Tracer Indicators for Maternal and Child Health and NTDs** | | |
| Mass Treatment Coverage for Neglected Tropical Disease (NTD index, %)(2023) | | 39 |
| % of Neglected Tropical Disease MDAs Achieving WHO Targets | | 40 |
| National Budget Allocated to NTDs | | |
| Estimated % of children (0–14 years old) living with HIV who have access to antiretroviral therapy (2024) | | 70 |
| DPT3 coverage 2024 (vaccination among 0-11 month olds) | | 83 |
| Climate Change and VBDs in NDCs | | |

Malaria imeenea katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukiwa na ongezeko kubwa (vilele) katika msimu. Taarifa ya Malaria ya mwaka 2023 imeonesha idadi ya wagonjwa ilikuwa 3,775,205 na vifo 2,002.

## Ufunguo:

- Lengo limefikiwa/utekelezaji unaendelea sawa
- Juhudi zaidi zinahitajika kufikia lengo
- Utekelezaji upo nje ya lengo
- Hamna takwimu
- Haihusiki

# Malaria

Bara la Afrika liko katikati ya dhoruba kali linalotishia kuvuruga utoaji huduma na kuathiri maendeleo yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa karne zilizopita. Nchi ni lazima kuchukua hatua za haraka ili kuzuia na kupunguza athari mbaya zinazoendelea kufuatia mgogoro wa kifedha duniani, kupungua misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea, kuongezeka kwa tishio la kibailojia, mabadiliko ya hali ya hewa na migogoro ya kibinadamu. Matukio haya yanatishia sana kuvuruga mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa malaria kwa takriban miaka 20, na huenda yakasababisha ongezeko la majanga na milipuko ya magonjwa, iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Ili kuwa na mwendelezo sahihi na hatimae kutokomeza kabisa malaria, zinahitajika dola bilioni 5.2 za kimarekani kila mwaka, ili kufadhili kikamilifu mahitaji ya mpango wa kitaifa wa malaria, na kujaza kwa haraka mapengo yaliyotokana na hivi karibuni kupungua kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea - ODA. Matukio ya hali ya hewa kali na mabadiliko ya hali ya hewa ni tishio kubwa kwa maendeleo yaliyopatikana. Afrika inakabiliwa na hatari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa na hadi kufikia mwaka 2030, watu milioni 150 zaidi watakuwa katika hatari ya kuugua malaria kwa sababu ya ongezeko la joto na kuongezeka kwa mvua. Majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa kali husababisha mamilioni ya watu kulazimika kuhama makazi yao, kuharibu miundo mbinu ya barabara na vituo vya huduma, na hivyo kupunguza njia ya kuvifikia vituo ili kupata huduma za afya. Nchi lazima zichukue hatua ya kukabiliana na tishio la usugu wa viuatilifu na usugu wa dawa za kutibu malaria, kupungua kwa ufanisi wa vipimo vya uchunguzi vinavyotoa majibu kwa haraka, na uwepo wa mbu vamizi aina ya *Anofelesi Stephensi* ambae anaeneza malaria katika maeneo yote ya mjini na vijijini.

Habari njema ni kuwa juhudi za kuboresha na kuongeza seti ya zana mbalimbali za kudhibiti malaria zinaendelea kupanuka. Shirika la Afya Duniani limeidhinisha matumizi ya vyandarua vipya venye aina mbili za viuatilifu zenye ufanisi mkubwa kwa zaidi ya asilimia 43, ukilinganisha na vyandarua vya kawaida, na matumizi ya vyandarua vipya yatasaidia sana katika kudhibiti athari za usugu wa viuatilifu. Dawa mpya za kutibu malaria na chanjo za malaria aina mbili kwa ajili ya watoto, tayari zimeidhinishwa na kuna ongezeko la idadi ya nchi za Afrika, ambazo zinatumia zana hizi mpya. Malaria inaweza kutumika kuonesha njia ya namna ya kuimarisha huduma ya afya ya msingi, mabadiliko ya hali ya hewa na afya, na huduma ya afya kwa wote. Nchi lazima zifanye kazi kuendeleza na kuongeza ahadi za rasilimali toka vyanzo vya ndani na kupitia sekta mbalimbali ikijumuisha vyanzo toka Mabaraza na Mifuko ya kutokomeza malaria na magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambapo hadi sasa imekusanya zaidi ya dola za kimarekani milioni 150.

## Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kufuatilia taarifa za makundi ya usugu wa viuatilifu tangu mwaka 2015, na kutoa taarifa kwa Shirika la Afya Duniani, na utaratibu wa kufuatilia viwango vya usugu, umesaidia katika kufanya maamuzi ya kuongeza usambazaji wa vyandarua vipya venye ubora na ufanisi zaidi, ili kukabiliana na usugu. Tanzania pia imeendelea na utaratibu wa kupima na kufuatilia usugu wa dawa za kutibu malaria, tangu mwaka 2018, na kutoa taarifa ya ufuatiliaji huo Shirika la Afya Duniani. Mpango mkakati wa taifa, umejumuisha afua mbalimbali zinazolenga pia kuwafikia wakimbizi. Tanzania pia inaonesha uongozi katika udhibiti wa malaria kupitia ushiriki wake kwenye mpango maalum kwa nchi zilizo na maambukizi makubwa ya malaria - HBHI, na hivi karibuni imetia saini Tamko la Yaonde. Tanzania pia imezindua Kampeni ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi. Sambamba na ajenda ya kipaumbele ya Mwenyekiti wa Muungano wa Viongozi wa Afrika katika Kudhibiti Malaria - ALMA, Mheshimiwa Rais, Wakili Duma Gideon Boko, nchi imeboresha mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji kwa malaria kwa kuandaa kadi ya alama ya kudhibiti na kutokomeza kabisa malaria, ingawa kadi ya alama bado haijashirikiwa kwa kitovu cha kadi ya alama cha ALMA. Nchi imezindua baraza na mfuko wa kutokomeza kabisa malaria.

## Matokeo:

Taarifa ya mwaka 2023, inaonesha kuwa idadi ya wagonjwa wa malaria ilikuwa 3,775,205 na idadi ya vifo vilivyotokana na malaria vilikuwa 2,002.

## Changamoto muhimu:

- Kudumisha ajenda muhimu ya utashi wa kisiasa na kutenga fedha kwa ajili ya Zanzibar, hasa ikizingatiwa kuwa maambukizi ya malaria visiwani humo yanaendelea kupungua.
- Rasilimali zisizotosheleza katika kutekeleza kikamilifu Mpango Mkakati wa Kitaifa wa malaria ikijumuisha athari za hivi karibuni za kupunguzwa kwa misaada ya maendeleo kwa nchi zinazoendelea.
- Kufuatilia tishio la uwepo wa usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu malaria.

## Utekelezaji wa mapendekezo muhimu yaliyopita:

| Lengo | Vipengele vya utekelezaji | Muda wa kukamilisha utekelezaji | Hatua ya Utekelezaji | Maoni - ufafanuzi wa shughuli/ mafanikio muhimu tangu ripoti ya robo mwaka iliyopita |
|---|---|---|---|---|
| Matokeo | Kufuatilia athari zinazotokana na Serikali ya Marekani kupunguza misaada kuhusiana na Mfuko wa Rais wa kushughulikia malaria - PMI, na kuzifanyia kazi ili kupunguza athari. | Robo ya 4 - 2025 | | Serikali imeainisha rasilimali toka vyanzo vya ndani ambazo zilijumuishwa katika bajeti ya mwaka huu ili kugharamia ununuzi wa bidhaa muhimu za malaria. Nchi kwa sasa inapitia mpango wa utekelezaji toka Mfuko wa Dunia na kuweka upya vipaumbele kwa rasilimali ili kuziba mapengo ya ufadhili. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matokeo | Kufanyia kazi kiwango kidogo cha vitendanishi vya malaria. | Robo ya 3 - 2025 | | Nchi kwa sasa ina akiba ya dawa mseto za kutibu malaria na vitendanishi ambavyo vinavyotosheleza matumizi zaidi ya miezi 6. |

## Huduma ya Afya ya Uzazi kwa Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto na Vijana.

### Hatua iliyofikiwa

Tanzania imefanikiwa kufikia kiwango cha juu kwenye kiashiria cha huduma ya afya ya uzazi kwa mama, mtoto mchanga, watoto na vijana katika ugawaji wa vidonge vya Vitamin A na Chanjo ya DPT3. Nchi imeimarisha kwa kiasi kikubwa mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji kwa kuandaa na kuzindua kadi ya alama yenye takwimu za afya ya uzazi, mama, mtoto mchanga, watoto na afya ya vijana, pamoja na utayarishaji wa kadi ya alama inayojumuisha sekta mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya lishe.

## Magonjwa ya kitropiki ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele.

### Hatua iliyofikiwa

Mafanikio ya kudhibiti magonjwa ya tropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yanapimwa kwa kutumia fahirisi ya kielezo kinachozingatia kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kwa magonjwa ya matende, usubi, kichocho, minyoo na trakoma.

Mwaka 2023, kiwango cha utekelezaji wa tiba-kinga kilikuwa asilimia 16 kwa udhibiti wa minyoo, asilimia 29 kwa udhibiti wa kichocho, asilimia 29 kwa udhibiti wa matende, asilimia 78 kwa udhibiti wa usubi, na asilimia 81 kwa udhibiti wa trakoma. Kiujumla kiwango cha utekelezaji kwa magonjwa ya tropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele kwa Tanzania kwa mwaka 2023 ni alama 39. Tanzania imefikia malengo ya Shirika la afya duniani kwenye ugawaji wa dawa-kinga kwa udhibiti wa usubi na trakoma pekee kwa mwaka 2023. Tanzania imeandaa kifungu katika bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa magonjwa ya kitropiki ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele.

## Utekelezaji wa mapendekezo muhimu yaliyopita:

| Lengo | Vipengele vya Utekelezaji | Muda wa kukamilisha Utekelezaji | Hatua ya Utekelezaji | Maoni - ufafanuzi wa shughuli/ mafanikio muhimu tangu ripoti ya robo mwaka iliyopita |
|---|---|---|---|---|
| Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Afya | Kazi ya kukusanya takwimu juu ya athari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa magonjwa yanayoenezwa na wadudu na kujumuishwa katika mzunguko wa awamu inayofuata ya michango kitaifa na mipango ya kitaifa ya mabadiliko ya hali ya hewa. | Robo ya 4 - 2025 | | Kwa sasa nchi inafanyia kazi ujumuishaji wa takwimu za hali ya hewa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Afya - ufuatiliaji na mwitikio wa magonjwa (HMIS-IDSR), hatimae itaunganishwa na mifumo mingine ili kutoa taarifa juu ya udhibiti wa magonjwa yanayoenezwa na wadudu, ikiwa ni pamoja na malaria katika muktadha wa ajenda pana zaidi inayohusu mabadiliko ya hali ya hewa.<br><br>Mkutano wa wadau husika ulifanyika katika robo ya 1 ili kuhakikisha kuwa takwimu za hali ya hewa zinajumuishwa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Afya - ufuatiliaji na mwitikio wa magonjwa (HMIS-IDSR). Kiolezo cha kidijitali kinapatikana kwa sasa ambacho kitajumuisha malaria na magonjwa mengine yanayoenezwa na wadudu katika muktadha wa ajenda pana ya mabadiliko ya hali ya hewa. |

### Ufunguo:

| | |
|---|---|
| (kijani) | Hatua iliyofikiwa |
| (njano) | Maendeleo yapo kiasi |
| (nyekundu) | Hamna maendeleo |
| (kijivu) | Bado muda wa matokeo |